**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS–TAMISEMI**

**Shule ya Sekondari**
**MPUI**

**S.L.P 338 SUMBAWANGA**

**Tarehe...................……………**

**Namba za Simu:-**

**Mkuu wa Shule: 0758432825**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0765817243**

**Matron: 0758063445**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA MPUI HALMASHAURI YA SUMBAWANGA MKOA WA RUKWA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya HGL

Shule ya Sekondari MPUI ipo umbali wa Kilometa 55 Mashariki mwa Mji wa Sumbawanga. Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi **Katumba** na nauli ni Shilingi 3,000/= kwa usafiri wa hiace

zinazoelekea mji wa Laela. Aidha kwa wale wanaotokea barabara ya Mbeya-Sumbawanga unapaswa kushuka kituo cha **Mpui ya UFIPA**.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**(a) Sare za Shule**

(i) Sare ya shule hii ni sketi mbili, Moja ya kijani iliyoiva (kitambaa kizito) na moja ya zambarau iliyoiva (kitambaa kizito). Sketi iwe ndefu inayofika chini na kugusa viatu. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.

(ii) Tai moja ya kijani iliyoiva na moja ya zambarau iliyoiva.

(iii) Rangi ya hijabu (kijuba) iwe nyeupe tu na ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

(iv) Sare ya Michezo kwa shule hii ni track suti rangi ya bluu bahari na raba za michezo jozi Moja.

(v) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

(vi) Soksi jozi mbili khaki.

(vii) Masweta mawili moja la kijani iliyoiva na moja la zambarau iliyoiva.

(viii) Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni magauni mawili mshono wa solo (bajaji) rangi ya pinki na iwe ndefu mpaka chini.

(ix) Tisheti (T-shirt) inapatikana shuleni kwa gharama ya TSH 10,000/=.

NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani nje ya maelekezo hapo juu na siku ya kuripoti avae sare za shule.

(b) **Mahitaji mengine muhimu**

i. Madaftari counter books 7 (3 quire)
ii. **Ream(A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka.
iii. Godoro moja
iv. Mashuka Jozi 2 rangi ya pinki, blanket 1, foronya ya godoro1, chandarua1.
v. Nguo za ndani za kutosha;
vi. Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe);
vii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
viii. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wandani na nje.

**(c) Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**b) Shule za Kutwa**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

**NB: Michango hii ilipwe kwenye akaunti 62102300244 MPUI SECONDARY SCHOOL.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizaraya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais–TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada yakuripoti shuleni. Mambo hayoni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule.

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana na mwanafunzi kwa mwanafunzi , kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3.3 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

4 . Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**PUDENSIANA JOHN KAMBOLE.**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NIVEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

- **Mkuuwashule 0758432825**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0765817243**
- **Mwandamizi Taaluma 0763441379**
- **Mwandamizi Malezi 0757216207**